Learning on TAP

# Upimaji wa uoni na usikivu kwa watoto wa umri wa shule

## Orodha ya vitu vya kuzingatia wakati wa upimaji

<table>
<tr><th colspan="3">Kabla ya upimaji</th></tr>
<tr><th colspan="3">Mahitaji ya upimaji — Mhusika: Mratibu wa upimaji</th></tr>
<tr><td>Idhini</td><td>Omba idhini kutoka Wizara ya Afya na Wizara ya Elimu</td><td>☐</td></tr>
<tr><td>Taratibu za Rufaa</td><td>Wasiliana na Mtoa huduma ya macho na masikio ili kujua taratibu za kupata rufaa. Angalia:<br>• Aina ya huduma wanayoweza kutoa<br>• Upatikanaji wa rufaa mpya<br>• Namna ya kupata rufaa<br>• Kama kuna namna unaweza kupata msaada wa kulipia gharama ua uasaidizi wowote</td><td>☐</td></tr>
<tr><td>Maeneo yanayofaa</td><td>Kutana na wakuu wa shule ili kuelezea programu na angalia kama vigezo vya upimaji vimefikiwa:<br>• Elezea sababu ya upimaji na shauri wafanyakazi wa shule watakahusika kwenye zoezi kusoma Moduli 1: Upimaji wa hisia kwa ajili ya watoto wenye umri wa kwenda shule<br>• Mahitaji ya nafasi ya upimaji:<br>  ○ Mahali panapofikika<br>  ○ Mwanga<br>  ○ Kelele<br>  ○ Urefu wa chumba<br>• Nyaraka zinazohitajika:<br>  ○ Fomu za ridhaa<br>  ○ Fomu za uchunguzi<br>  ○ Fomu za kutoa taarifa<br>  ○ Ufuatiliaji wa vitu vinavyohitajika kwa ajili ya rufaa<br>  ○ Dondoo za kuwa na macho na masikio yenye afya bora<br>  ○ Orodha ya vitu vinavyohitajika kwa ajili ya upimaji shuleni/ jedwali maalum<br>• Wafanyakazi wanaohitajika:<br>  ○ Mratibu wa upimaji wa shuleni<br>  ○ Wasaidizi kwa ajili ya kupanga na kusindikiza watoto pale inapotakiwa<br>• Mchakato wa ridhaa na makubaliano na mzazi/melzi/mkuu wa shule pamoja na nyaraka zinazotakiwa<br>• Maelezo ya siku ya upimaji, ikiwemo vipindi vya vikundi mbali mbali<br>• Taratibu za siku ya upimaji, kupanga na kusimamia watoto. Je, kuna mtoto mwenye mahitaji maalum?</td><td>☐</td></tr>
<tr><th colspan="3">Matayarisho ya upimaji — Wahusika: Mratibu wa upimaji na mratibu wa shule</th></tr>
<tr><td>Orodha ya vitu vinavyotakiwa: Nyaraka</td><td>Wasiliana na shule kuhusu:<br>• Kuhakikisha kuwa fomu za ridhaa zinawekewa sahihi na kujazwa tayari kwa siku ya upimaji na kukamilishwa kwa rufaa ya kila mtoto<br>• Kukamilisha Orodha ya upimaji ya shule<br>  ○ Uwepo wa fomu tupu za upimaji, Fomu za kutoa taarifa na orodha ya vitu vinavyohitajika katika ufuatiliaji wa rufaa<br>• Eneo la upimaji ni saafi na sehemu ya kukaa iko tayari</td><td>☐</td></tr>
<tr><td>Orodha ya vitu</td><td>Wasiliana na mratibu:</td><td>☐</td></tr>
</table>

| | | |
|---|---|---|
| **vinavyotakiwa:** Vifaa | • Kuainisha na kukagua kifaa kupima uoni na kusikia- angalia kama nafasi ya kufanya kipimo tayari imepangwa<br>o Kuna bateri na taa za ziada kwa ajili ya Kifaa cha kupima kusikia na tochi ya kalamu/ Kifaa cha kupima uoni | |

| | | |
|---|---|---|
| **Siku ya upimaji** | | |
| **Kabla ya shughuli za upimaji** | **Wahusika: Wapimaji/Mratibu wa shule** | |
| **Kuandaa mahali pa kufanyia upimaji** | **Andaa eneo na vifaa vya upimaji:**<br>• Angalia kama kuna kelele iliyokuzunguka kwa kutumia mita maalum ya kupima kiwango cha sauti au tumia simu, yenye kitufe cha kuangalia kiwango cha sauti. Usiendelee kufanya kipimo kama sauti itazidi 40dB<br>• Sehemu ya kukaa:<br>o Viti viwili<br>o Meza<br>• Vipimo vya upimaji macho:<br>o Chati za HOTV<br>o Kadi maalum za kuonyesha<br>o Chati za E<br>o Kizibo cha jicho (optional)<br>o Utepe wa kupimia<br>o Tochi ya kalamu/ Kifaa cha kupima uoni<br>o Utepe<br>o Vitu vya usafi vya mikono na vifaa<br>• Vifaa vya kupima usikivu:<br>o Mita ya kupima kiwango cha sauti<br>o Adiomita (mashine au programu ya kwenye simu)<br>o Kifaa cha kupima usikivu<br>o Kifaa cha kutanua sikio “Spekulamu” (walau viwili vya ukubwa tofauti)<br>o Vitu vya usafi wa mikono pamoja na vifaa | ☐ |
| **Kipindi cha Kikundi** | **Simamia vipindi vya vikundi**<br>• Uelewa wa afya ya macho na masikio kwa watoto wote<br>• Maandalizi ya vipimo kwa watoto ambao wamepata ridhaa ya kupimwa | ☐ |
| **Upimaji wa uoni na afya ya macho** | **Wahusika: Wapimaji** | |
| **Hatua ya 1:** Kuwa tayari | • Hakikisha kuwa una fomu ya ridhaa sahihi<br>• Nakili majibu kutoka kwenye maswali ya awali kabla ya upimaji kwenye fomu ya upimaji isiyokuwa na kitu chochote<br>• Angalia kama mtoto amevaa miwani kama anaitumia ili kuweza kuona mbali. | ☐ |
| **Hatua ya 2:** Upimaji wa uoni wa mbali | **Fanya upimaji wa uoni:**<br>1. Safisha kizibo cha macho (kama kuna kizibo unachotumia)<br>2. Chagua chati sahihi:<br>o Watoto wenye umri wa miaka 8 au pungufu wanatumia chati ya HOTV na kadi ya kuonyesha<br>o Watoto wenye umri zaidi ya miaka 8 wanatumia chati ya E<br>3. Kaa na mtoto kwa umbali wa mita 3 kutoka kwenye chati iliyo kwenye ukuta<br>4. Mwelezee mtoto utaratibu wa upimaji: | ☐ |

| | | |
|---|---|---|
| | ○ Chati ya HOTV -Onyesha herufi zinazofanana kwa kutumia kadi ya kuonyesha<br>○ Chati E- inaonyesha uelekeo wa herufi E<br>5. Pima jicho la kulia halafu pima la kushoto<br>6. Ziba taratibu jicho ambalo halipimwi kwa kutumia kiganja cha mkono au kizibo cha jicho<br>7. Pitia fomu ya upimaji. Weka kumbukumbu ya majibu ya kila jicho na majibu kwa ujumla | |
| **Hatua ya 3:**<br>Upimaji wa afya ya macho | **Tayarisha na fanya upimaji wa afya ya macho:**<br>8. Osha kwa sabuni au kitakasa mikono na ikaushe<br>9. Mwelezee mtoto kuwa utaangalia ndani ya macho yao kwa kutumia tochi<br>10. Kagua kila jicho kwa kutumia tochi<br>11. Weka kumbukumbu ya matokeo | ☐ |
| **Upimaji wa kusikia na afya ya masikio** | | **Wahusika: Wapimaji** |
| **Hatua ya 1:**<br>Kuwa tayari | • Kagua kama una fomu ya ridhaa sahihi na nakiri taarifa yoyote inayokosekana kwenye fomu ya upimaji<br>• IKama mtoto anatumia vifaa saidizi vya kusikia, anapaswa kuvitoa kwa ajili ya upimaji wa usikivu<br>• Angalia kama kiwango cha kelele sawa, kwa kutumia kipimo cha kiwanog cha sauti/ mfumo wa kwenye simu. Usiendele kama kiwango cha sauti ni zaidi ya 40dB. | ☐ |
| **Hatua ya 2:**<br>Vipimo vya kusikia | **Fanya vipimo vya kusikia:**<br>1. Mkalishe mtoto kwenye kiti.<br>2. Mwelezee mtoto utaratibu wa upimaji wa usikivu:<br>○ Mtoto atasikia sauti kupitia spika za masikioni<br>○ Kila mara wanaposikia sauti, wakuonyeshe upande sauti inaposikika. Kwa mfano, kwa kuinua mkono wao wa kulia au kushoto.<br>3. Mvalishe mtoto spika za kwenye masikio. Hakikisha spika za maskioni zimefunika masikio na hazimfanyi mtoto kujisikia vibaya.<br>4. Pitia vipengele vyote vilivyo kwenye fomu ya upimaji na weka kumbukumbu ya matokeo ya kila sikio | ☐ |
| | **Jaribu kupima : 1000Hz kwenye 40dB**<br>1. Weka masafa ya sauti ya 1000Hz, na kuongeza sauti hadi 40dB<br>2. Ongeza sauti kwenye sikio la kulia:<br>○ Kama mtoto ataonyesha kuwa anasikia sauti hiyo, andika jibu la kufaulu kwenye sikio hilo.<br>○ Kama mtoto hatajibu, jaribu tena, mara mbili tu.<br>○ Kama mtoto hajibu kwa mara ya pili au ya tatu, andika chini ☞ Rejea matokeo ya sikio hilo<br>3. Rudia tena mchakato huu kwa sikio la kushoto<br>Matokeo:<br>• Kama mtoto haonyeshi kuwa anasikia sauti baada ya kujaribisha mara tatu kwa sikio moja au masikio yote mawili, usiendelee na upimaji wa usikivu ☞Rejea jedwali la matokeo yaliyo kwenye fomu ya upimaji na anza upimaji wa afya ya m asikio<br>• Kama mtoto ameonyesha usikivu wa sauti kwenye masikio yote mawili, kwenye moja ya majaribio matatu yaliyofanyika, endelea. | ☐ |
| | **Upimaji wa usikivu: 1000Hz, 2000Hz na 4000Hz kwenye 20dB**<br>• Hakikisha mtoto haoni audiomita iliyo mikononi mwako wakati unapima kipimo cha usikivu. | ☐ |

| | | |
|---|---|---|
| | 1000Hz kwenye 20 dB:<br>1. Weka masafa ya sauti kwenye 1000Hz na punguza sauti hadi kiwango cha 20dB.<br>2. Fanya hivi mara tatu kwa sikio la upande wa kulia<br>3. Tunza kumbukumbu ya majibu vipimo ya mtoto kwa kuweka alama ya vema (✓) au Mkasi (X) kwenye fomu ya upimaji kwa kila sikio<br>4. Rudia mchakato wa hapo juu kwa sikio la upande wa kushoto<br>2000Hz kwenye 20dB:<br>5. Rekebisha viwango na rudia mchako ule ule kama hapo ju.<br>4000Hz kwenye 20dB:<br>6. Rekebisha viwango na rudia mchako ule ule kama hapo ju.<br>7. Rekodi matokeo ya kila sikio na majibu ya jumla | |
| **Hatua ya 3:** Upimaji wa afya masikio | **Tayarisha na fanya upimaji wa afya ya masikio:**<br>• Osha mikono na ikaushe. Tumia sabuni/ vitakasa mikono.<br>• Tumia kemikali maalum ya kuua vijidudu kwenye kitanua maskio (spekulamu)<br>• Mwelezee mtoto kuwa utakuwa unaangalia kwenye sikio lake kwa kutumia kifaa cha kupima usikivu (otoskopu) | ☐ |
| | **Kagua 1: Sehemu ya nje ya sikio**<br>1. Kagua nje ya sikio kutoka nyuma kwenda mbele.<br>2. Andika chini majibu.<br>3. Bonyeza taratibu sehemu ya nje ya sikio ambayo ipo karibu na njia iitwayo “tragus” ili kuona kama kwa kufanya hivi mtoto anasikia maumivu. Maumivu yanaweza kuwa dalili ya maambukizi<br>4. Kama mtoto anasikia maumivu unapobonyeza sehemu hii ya sikio, sitisha zoezi la upimaji na weka kumbukumbu ☞ Rejea kwenye jedwali la majibu. Waweza pia, Kuendelea. | ☐ |
| | **Kagua 2: Njia ya sikio (canal)**<br>5. Shika kifaa cha kupima kusikia kwa mkono ulioko upande ule ule wa sikio la mtoto. Vuta sikio ili kufungua njia ya sikio.<br>6. Andika chini matokeo ya kila sikio<br>Matokeo:<br>• Kama hakuna dalili zozote za matatizo ya kiafya kwenye sikio lolote, andika kuwa mtoto amefaulu kipimo<br>• Kama kuna dalili zozote za matatizo ya kiafya ya sikio,andika ☞ Rejea matokeo ya kipimo. | ☐ |
| **Programu ya Upimaji** | | **Wahusika: Wapimaji** |
| **Hakuhudhuria** | **Kama mwanao hakuhudhuria upimaji:**<br>Panga siku ya kurudi kufanya vipimo siku nyingine | ☐ |
| **Amefaulu** | **Kama mwanao amefaulu vipimo vyote:**<br>• Kama hakuna dalili ya shida zozote za uoni na kusikia,kusudia kuwajulisha wazazi wake kwa kutumia fomu ya kutoa taarifa<br>• Kama mzazi/mlezi ana dukuduku, kusudia kujadili na wazazi na kufanya upimaji | ☐ |
| **Rufaa:**<br>Mtaalam wa huduma ya macho | **Ainisha mpango wa kumuona mtaalam wa macho kwa kila ☞ Rejea matokeo yaliyopatikana kutokana na:**<br>• Maswali kabla ya kufanya upimaji<br>• Upimaji wa uoni wa mbali | ☐ |

| | | |
|---|---|---|
| | • Upimaji wa afya ya macho | |
| **Rufaa:**<br>Mtaalam wa masikio | **Ainisha mpango wa kumuona mtaalam wa masikio kwa kila ☞ Rejea matokeo yaliyopatikana kutokana na:**<br>• Upimaji wa usikivu<br>• Upimaji wa afya ya masikio | ☐ |

| **Baada ya shughuli za upimaji** | **Wahusika: Wapimaji na mratibu wa shule** | |
|---|---|---|
| **Nyaraka** | • Hakikisha fomu zote za upimaji zimekamilika<br>• Ongeza maelezo kwenye vitu vya kufuatiliwa kwa ajili ya rufaa<br>• Ongeza maelezo kwenye orodha<br>• Boresha kumbukumbu kuhusu shule:<br>  o Mahudhurio<br>  o Matokeo ya waliofaulu vipimo<br>  o Matokeo ya waliopewa rufaa<br>  o Ufuatiliaji wa upimaji | ☐ |
| **Vifaa na eneo la upimaji** | Safisha vifaa na nafasi ya kufanya vipimo | ☐ |

| **Baada ya siku ya upimaji** | | |
|---|---|---|
| **Mawasiliano na utunzaji wa kumbukumbu** | **Wahusika: Mratibu wa upimaji na mratibu wa shule** | |
| **Mawasiliano na wazazi** | • Hakikisha shule ina nakala ya orodha ya vitu vya kufuatilia kwa ajili ya rufaa<br>• Shule:<br>  o Ongea na wazazi/walezi wa watoto wanaohitaji rufaa<br>  o Tuma kwa wazazi wote; fomu ya taarifa na taarifa kuhusu namna macho yenye afya bora yanapaswa kuwa.<br>  o Fuatilia mahudhurio ya waliopewa rufaa wakati wanapokuja kwenye rufaa zao<br>  o Panga siku nyingine ya upimaji au weka mpango unaojumuisha watoto wote ambao hawakuweza kuhudhuria<br>• Pendekeza siku ya kurudi kupimwa ndani ya mwezi mmoja kama wazazi/lwalezi wana dukuduku hata kama mtoto atakuwa alifaulu siku alipopimwa | ☐ |
| **Mawasiliano na mtaalamu wa macho na masikio** | • Wasiliana na mtaalam atakayepokea rufaa na kumjulisha kuhusu idadi ya rufaa ambazo atarajie kutoka kwako<br>• Kama mtoto tayari anatumia vifaa saidizi vya uoni na kusikia, wasiliana na pale anapopata huduma hiyo | ☐ |
| **Mawasiliano na shule** | Fuatilia shuleni ili:<br>• Kuangalia kama mahudhurio kwenye sehemu watoto wamepewa rufaa yapo kweli<br>• Pendekeza siku nyingine za kufanya vipimo | ☐ |
| **Utunzaji kumbukumbu** | • Hakikisha unaboresha orodha ya mambo ya kufuatilia kwa ajili ya rufaa<br>• Tunza kumbukumbu na toa taarifa ya kumbukumbu za usimamizi na tathmini kama | ☐ |

| | | |
|---|---|---|
| | ilivyokubaliwa. | |